

IOFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI ALENI,
S. L. P. 252,
MKUU – ROMBO.
17/12/2020

Kumb.NA.ASS/ADM/F.I/2021

KWA _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ALENI; WILAYA YA ROMBO MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. **HONGERA.** Shule ya sekondari Aleni ipo umbali wa km 15 kutoka mji mkuu wa halmashauri ya wilaya ya Rombo .

Muhula wa kuanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2020**. Unatakiwa kuripoti shulenii tarehe **11/01/2021** saa 2:00 asubuhi ukiwa na Mzazi/Mlezi wako

2.0 Mambo muhimu yakuzingatia

2.1 Sare za shule

Sare ya shule hii ni :

a) WAVULANA

Suruali mbili rangi ya **DARK BLUE**, mashati mawili meupe mikono mifupi, sweta rangi ya **DARK BLUE** , Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba, tai ya rangi ya **DARK BLUE**.

b) WASICHANA

Sketi mbili rangi ya **DARK BLUE**, mashati mawili meupe mikono mifupi , sweta rangi ya **DARK BLUE**, soksi ndefu nyeupe, tai rangi ya **DARK BLUE** na viatu nyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba.

Mashono

Kila mzazi/mlezi amshone mwanae suruali , sketi, shati, sweta na tai kwa kufuata maelezo yafuatayo:

1. Suruali isiwe **MLEGEZO**, iwe na mifuko mitatu, marinda mawili (**celebration**) na iwe na mikunjo chini (**pindo**). Isiwe ya kubana yaani modo. Mifuko ya **SIMPLE** hairuhusiwi.
2. Sketi lazima iwe ndefu ifike kwenye kiwiko cha mguu wa wanafunzi na iwe na marinda 12 na siyo Box.
3. **USISHONE SARE YENYE MIFUKO YA KIHUNI**. Atakayefika shulenii na sare isiyokubalika atarudishwa nyumbani.

c) Sare ya michezo kwa shule hii ni

T-sheti ya rangi ya DARK BLUE na bukta yenyeye mistari ya rangi nyeupe na kijani kwa wavulana na kwa wasichana.

2.2 Daftari kubwa counter books **tisa (9)** kuanzia Quire 2, kalamu za kutosha, mkebe wa hesabu, Rula,penseli na **dictionary** (kamusi ya kingereza)

2.3 Chakula cha wanafunzi kitagharamikiwa na mzazi kutokana na makubaliano ya kikao cha wazazi

2.4.Matibabu ya wanafunzi yataghalamikiwa na mzazi.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu **Na 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na 10** ya mwaka **1995**. Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundu , yenyeye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya waziri mkuu- TAMISEMI yenyeye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa:
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
- h) Kutunza mali za umma.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

- a) wizi
- b) uasherati na ushoga
- c) ubakaji
- d) ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli/ugoro na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa
- h) Kuwa mjamzito au kupata mimba.
- i) Kuoa au kuolewa
- j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi
- l) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulenii na mwanafunzi.

- a) ‘Medical Examination Form’ ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.
- b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 .Tafadhali soma kwa **makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
**NADE B. NAWE
MKUU WA SHULE.**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
SHULE YA SEKONDARI ALENI
SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE**

Ili shule iweze kuendesha shughuli za kila siku ni lazima kuwa na aina fulani ya utaratibu, kanuni na sheria za shule. Yote haya yanalenga katika malezi na madhumuni ya wewe mwanafunzi kuwepo hapo shulenii kwa mujibu wa maadili ya Taifa. Mwanafunzi anatakiwa afahamu; azingatie na afuate yafuatayo.

- i. Kuwa na heshima na adabu. Shule ni mahali pa malezi ya vijana wa Taifa hili wanafunzi wote lazima waonyeshe heshima na adabu kwa wakubwa na viongozi wote bila kujali rangi, hali, kazi, n.k. mwanafunzi anapozungumza na mkubwa au kiongozi lazima asimame kwa adabu na awe mtulivu. Ni kosa kwa mwanafunzi kuzungumza na kiongozi wa aina yejote akiwa ameweka mikono mfukoni, anayumbayumba au kuegemea kitu kama meza, kiti au ukuta.
- ii. Kuongea lugha safi isiyo na matusi wala kashfa kwa binadamu yejote.
- iii. Kushiriki na kusaidia kazi za shule.
- iv. Kuwahi shule, kufanya kazi zote za shule kuendana na maagizo yatolewayo na uongozi wa shule.
- v. Kuhakikisha kwamba mazingira ya shule/ unakoishi yanakuwa safi wakati wote kwa kufanya usafi.
- vi. Kusimama na kusalimia wakubwa wanapopita mbele yako.
- vii. Kuheshimu Bendera ya taifa letu, wimbo wa Taifa , wimbo wa shule , Nembo ya Taifa , Picha za viongozi wa serikali n.k.
- viii. Kupokea kwa heshima mizigo kwa watumishi wa shule, na wageni wa shule na kuwasaidia.
- ix. Kusimama na kusalimia kwa heshima mwalimu/walimu mara tu aingiapo /waingiapo darasani.
- x. Kutii na kuheshimu wito wowote unaotolewa shulenii.
- xi. Kuheshimu mahali pa mikusanyiko kwa utulivu na kufuata utaratibu uliowekwa.
- xii. Kushiriki pamoja na wanafunzi chakula kitolewacho hapa shulenii wakati wa mchana kwa siku zote za masomo.
- xiii. Kusoma kwa bidii na kufanya mazoezi na mitihani yote inayotolewa shulenii, wilayani, kanda na taifa.
- xiv. Kuwasilisha hati za malipo ya fedha (Pay in Slip) na michango mingine ya shule kwa wakati mwafaka ofisi ya mkuu wa shule.
- xv. Unatakiwa kuwepo hapa shulenii saa **1:00 asubuhi** hadi saa **10:30 jioni** kwa siku zote za masomo.

2.MAKOSA AMBAYO HAYARUHUSIWI MWANAFUNZI KUYATENDA (MIIKO)

Mwanafunzi atakeyepatikana na kosa kati ya haya yaliyoorodheshwa hapa chini atafutwa shule mara moja.

- i. Kashfa za aina yoyote kwa Taifa na viongozi wa Taifa kama kudharau mambo ya kitaifa.
- ii. Wizi/kuiba
- iii. Kufunga ndoa ukiwa bado mwanafunzi, ubakaji, uasherati, kumpa/kupata mimba, kujaribu au kushawishi kutoa mimba, ushoga.
- iv. Kuharibu mali ya shule/binafsi.
- v. Kutohudhuria shule kwa muda mrefu (utoro) bila taarifa.
- vi. Kumtishia , kumpiga mwalimu au kiranja yeyote wa shule au kupigana.
- vii. Kunywa pombe ya aina yoyote, matumizi ya madawa ya kulevya na kuvuta sigara.
- viii. Kuendesha biashara, magesdo au ulangazi wa aina yoyote.
- ix. Kosa la jinai, kosa lillothibitishwa na polisi, uwe umefikishwa mahakamani.
- x. Kugoma adhabu, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu.
- xi. Kukataa adhabu, kutoheshimu watu wenyewe mamlaka dhidi yako na kufanya vikao visivyo halali.
- xii. Kutofanya mazoezi ya mitihani ya shule, wilaya, kanda na Taifa.
- xiii. Kutokula chakula kitolewacho shuleni (idhini inatolewa kwa maandishi na **(MKUU WA SHULE)** tu kutokana na ushauri wa daktari mkuu wa Hospitali au kituo cha Afya cha serikali.
- xiv. Kukutwa na vifaa vya muziki, Radio na Simu za mikononi katika mazingira ya shulena hata nje ya shule .

3. MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUYATENDA.

Mwanafunzi awapo shuleni au nje ya shule hataruhusiwa kutenda mojawapo ya yafuatayo:- kutenda au kujaribu kushawishi kutenda ni kwenda kinyume na hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake na uongozi wa shule na ikiwezekana wazazi/walezi wake watashirikishwa.

- i. Kutumia tumbaku au ulevi wa aina yoyote ile.
- ii. Kuвая mavazi yasiyo ya heshima.
- iii. Kufuga kucha ndefu na kuвая hereni, mikufu n.k na kuвая mavazi yasiyo ya heshima
- iv. Kuiga mitindo ya kihuni kama kunyoa kipara, panki, kupiga picha za kihuni kupaka midomo rangi na kucha, marashi, n.k.
- v. Kutumia lugha ya matusi au kashfa.
- vi. Kutoroka vipindi darasani.
- vii. Kutoroka nje ya eneo la shule bila ruhusa kwa mwalimu mhusika.
- viii. Kutembelea maeneo ya starehe kama vilabu vya pombe, nyumba za wagoni, kumbi za starehe, makazi ya watumishi, ofisi za walimu, stoo za shule, jikoni, maabara n.k bila ruksa .
- ix. Kutegea kazi za mikono .

Lengo kuu ni kutaka kila mwanafunzi awe na jitihada kubwa katika kufanya kazi na shughuli zote ndani na nje ya shule kwa bidii na nguvu zake zote. Atumie maarifa katika mambo . hivyo mwanafunzi anatakiwa atumie akili na maarifa kwa kila afanyalo kwa manufaa yake , shule, jamii na taifa kwa ujumla

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI ALENI
(Ijazwe kwa herufi kubwa irejeshwe ofisi ya kujiandikisha shulen)

1. Jina kamili la mwanafunzi _____
2. Tarehe ya kuzaliwa _____
3. Mahali alipozaliwa _____
4. Shule alikomaliza darasa la saba _____
5. Uraia wake _____
6. Dini yake _____ Dhehebu lake _____
7. Jila kamili la mzazi/mlezi

a) Kijiji/mtaa anakoishi _____
b) Kazi ya mzazi wake /mlezi _____
c) Anwani yake _____
d) Namba ya simu _____

MKATABA NA KAULI YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII

1. MWANAFUNZI

Mimi _____ (Jina la mwanafunzi) . ninakiri kuwa nimesoma na kuelewa yote kwenye maagizo ya kujiunga na shule hii na nitayazingatia kwa muda wangu wote wa masomo yangu hapa shulen Aleni. Aidha naahidi kukubali maagizo yote nitakayopewa na shule. Endapo nitakiuka na kwenda kinyume na taratibu, kanuni na sheria za shule hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

.....
Saini ya mwanafunzi

.....
tarehe.

2. MZAZI/MLEZI

Mimi _____ (jina kamili) ambaye ni mzazi mlezi wa _____ (jina la mtoto anayejiunga na shule hii)
ninakiri kupokea , kusoma na kuzielewa taratibu zote zilizoko kenyé maagizo ya kujiunga na sekondari ya Aleni. Iwapo mwanangu atakiuka taratibu hizo nitakuwa tayari kukubali hatua zitakazochukuliwa dhidi ya mwanangu anayejiunga na shule hii.

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI

TAREHE.

PRIME MINISTER'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
ALENI SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM

TO be completed by a medical officer in a government hospital in respect of all new entrants to Aleni secondary school.

Full name _____

Age _____

1. Blood count (red& white) _____

2. Stool examination _____

3. Urine examination _____

4. Eye test _____

5. Ear test _____

6. Speech test _____

7. T.b test _____

8. Std' stest _____

9. Spleen _____

10. Abdomen _____

11. Addition information from any physical, mental, hereditary diseases or disability _____

Treatment after examination _____

Please state nature of treatment _____

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above mentioned been examined by me and found fit/unfit to persue further education.

Signature _____

Designation/Stamp _____

Date _____ Station _____